*Tangazo hili limeidhinishwa na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA)*

**CRDB BANK PLC**

(Imesajiliwa nchini Tanzania chini ya Sheria ya Kampuni ya Tanzania namba 212 ya mwaka 2002 kama kampuni yenye dhima ya ukomo, cheti cha usajili namba 42094)

# TANGAZO KWA UMMA
# MATOKEO YA MAUZO YA HATIFUNGANI YA MIUNDOMBINU YA SAMIA (SAMIA INFRASTRUCTURE BOND)

CRDB Bank PLC ("CRDB") inatoa taarifa kwa umma kuwa mnamo tarehe 11 Oktoba 2024, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) katika kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, Sura ya 79 ya Sheria za Tanzania, ilitoa idhini kwa benki ya CRDB kuuza Hatifungani ya Miundombinu ya Samia (Samia Infrastructure Bond) yenye thamani ya shilingi bilioni 150 (TSH. 150,000,000,000), ikiwa ni toleo la pili la Programu ya Hatifungani ya miaka 5 yenye jumla ya shilingi za Kitanzania sawa na Dola za Marekani Milioni 300.

## MATOKEO YA MAUZO YA HATIFUNGANI

Mauzo ya Hatifungani ya Miundombinu ya Samia yalifunguliwa Ijumaa, tarehe 29 Novemba 2024 na kufungwa Ijumaa, tarehe 17 Januari 2025, ambapo kiasi cha shilingi bilioni 323.09 kimepatikana, ikilinganishwa na shilingi bilioni 150 zilizotarajiwa kupatikana, sawa na mafanikio ya asilimia 215.4.

## MUHTASARI WA MAUZO

Muhtasari wa takwimu muhimu za mauzo ni kama ifuatavyo:

| | |
|---|---|
| Mtoaji | CRDB Bank PLC |
| Maelezo | Hatifungani ya Miundombinu ya Samia |
| Muda | Miaka 5 |
| Aina ya Hatifungani | Daraja la kwanza, isiyokuwa na dhamana |
| Tarehe ya Kutoa | 10 Februari 2025 |
| Jumla ya kiwango kilichotolewa | TSH 150,000,000,000 (Shilingi za Kitanzania Billioni Mia Moja na Hamsini tu) |
| Kiasi kilichokusanywa | TSH 323,090,000,780 (Shilingi za Kitanzania Bilioni Mia Tatu Ishirini na Tatu, Milioni Tisini, Mia Saba na Themanini) |
| Kiwango cha matokeo (%) | 215.4 |
| Jumla ya kiasi kilichokubaliwa | TSH 323,090,000,780 |
| Bei ya Hatifungani | Ni ile iliyotangazwa |
| Kiwango cha chini cha Uwekezaji | TSH 500,000 (na nyongeza ya mafungu ya 10,000) |
| Riba iliyopangwa (Kuponi) | 12.00% kwa mwaka inayolipwa kila robo mwaka |

| | |
|---|---|
| Matumizi ya fedha zilizopatikana | Fedha zilizopatikana zitatumika kuwawezesha wakandarasi wa ndani ambao wanafanya kazi na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini Tanzania (TARURA) kuwa na uwezo wa kifedha ili kutekeleza kwa ufanisi na wakati miradi ya ujenzi wa miundombinu ya barabara vijijini na mijini hapa nchini. |

**SERA YA UGAWAJI**

Kutokana na mafanikio ya mauzo ya Hatifungani ya asilimia 215.4, CRDB Bank PLC imeomba na kupata idhini kutoka CMSA ya:

i. Kutumia kiasi chote cha fedha kilichopatikana kupitia mauzo ya Hatifungani ya Miundombinu ya Samia; na
ii. Kukubali maombi yote sahihi yaliyopokelewa kufikia kiasi cha shillingi 323,090,000,780. Wawekezaji wote watapokea asilimia mia (100%) ya maombi yao kwa mujibu wa Sera ya Ugawaji.

**MAELEZO YA ZIADA**

Endapo mwekezaji katika Hatifungani hii atahitaji ufafanuzi, anashauriwa kuwasiliana na Wakala wa Soko la Hisa au CRDB Bank PLC kupitia info@crdbbank.co.tz au +255(22)2197700)

**TAREHE ZA MATUKIO MUHIMU**

Tafadhali zingatia tarehe zilizopendekezwa kufuatia ufungaji wa ofa:

| Maelezo | Tarehe |
|---|---|
| Tarehe ya kutaarifiwa (kupitia baruapepe/ simu) | Jumatatu 10 Februari 2025 |
| Tarehe ya toleo | Jumatatu 10 Februari 2025 |
| Tarehe ya Kuiva kwa Hatifungani | 10 Februari 2030 |
| Tarehe ya Malipo ya Riba | 10 Mei, 10 Agosti, 10 Novemba na 10 Februari, |
| Tarehe ya kuorodheshwa hatifungani kwenye soko la hisa | Jumanne 18 Februari |

**SHUKRANI**

Menejimenti ya CRDB inatoa shukrani za dhati kwa taasisi zote zilizofanikisha uuzwaji wa hatifungani ya Miundombinu ya Samia. Taasisi hizi ni pamoja na Bodi na Uongozi wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA); Bodi na Uongozi wa Soko la Hisa la Dar Es Salaam (DSE); Mshauri Kiongozi katika utoaji wa Hatifungani hii, iTrust Finance Limited na Stanbic Bank; Dalali Mfadhili, iTrust Finance Limited na Orbit Securities Co Ltd; pamoja na Washauri wa Masuala ya Kisheria, Dentons EALC East Africa Law Chambers.

**Imetolewa na:**
**Afisa Mtendaji Mkuu,**
**CRDB Bank PLC**
**Plot No. 25, 26 Ali Hassan Mwinyi Rd,**
**S.L.P 268, Dar es Salaam,**
**Tanzania**

**Tarehe: 18 Februari 2025**

Tangazo hili limetolewa kwa idhini ya Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana kwa mujibu wa kanuni za Mamlaka za Matangazo, G.N. Namba. 15 ya mwaka 1997.